# DROIT CANONIQUE

## DE L’ EGLISE ORTHODOXE

### MU LUGHA KISWAHILI


**CENTRE DE MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI KONGO**
**1996**

# MWANZO

Droit (Sheria) ni nini?

Ni kundi ya usawa na ya Kanuni. Kazi yake ni kutengeneza uzima wa watu na matengeneo ya jamii.

Droit (Sheria) ya Kanisa: Ni Kanuni ya shina la fundisho ya Bwana Yesu Kristu na makutano ya mataguso kubwa.

Kanuni inatuasaidia sisi kupata uzima mzuri ya kiorthodoksi; na unatusaidia bila kufanya kosa mbele ya Kanisa ao zambi iko natuchunga namna ya sisi kuwa na uzima ya kiroho ndani ya Kanisa na kupata wokovu wetu.

-Inatusaidia sisi wa Kristu kuungana sawa mwili moja wa Yesu Kristu.

-Inatuchunga kwa kuepuka ma kanisa heretique (Wa uwongo) na kukataa fundisho ingine ya hatari.

Magumu katika kanuni ya jamii na ya Kanisa na hii:

a) Kanuni ya jamii ni uwezo kwa watu (kupenda ao hapana ya faa kufuata mstari wa jamii kama apana ndani ya gerezani.

b) Kanuni ya Kanisa ni uhuru sawa vile Kristo anasema: «Hule anapenda kunifwata abebe Msalaba wake.

MWANZO (origine): Siku ya kwanza ya Kanisa yetu ni siku ya Pentikosti (Historia ya Eklezya (Juma ya Pentikosti).

-Mwanzo ya kazi ya Kanisa ni kuwa Missionaire (Yesu Kristu anasema: «Endeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu» (Matayo 28, 18-20).

Tangu ile wakati fundisho ya Bwana Yesu Kristu ilisambazwa fasi yote na kufanya Kanisa.

Kanisa ni nini? Ni kiwili wili moja Takatifu ile Bwana Yesu Kristu alijenga juu ya kuponyesha watu.

Kanisa hii ni yenye kujaa, ambamo watu wote wenye kuamini Kristu wajikusanye mara moja na wamufwate Bwana Yesu Kristu na Mitume zake.

Bwana Yesu Kristu analeta uwezo wake kwa Mitume. Kanisa ni maugano. Na tena Kristu na Kanisa ni maungano, hivi kwetu sisi ni kupata wokovu.

1) Kanisa ni moja: Kwa sababu umoja ni Kichwa cha Bwana Yesu kristu na mwili moja.

2) Mukubwa wa Kanisa ya Yesu Kristu ni Mutakatifu, naye alitakasa Kanisa kwa ajili ya damu yake Takatifu, kwa neema yake kila mwaminifu (membre) wa Kanisa anatakasa kama anapenda.

3) Katholique (Wa dunia muzima na fundisho muzima). Hii neno inatokea ya lugha kigreki. Maana ya hii neno ni hii:

1)Fundisho yake ni muzima;

2)Kazi yake ni juu ya kuzambaza habari ma fasi zote.

4) Kanisa ni Apostoliki (Wa Mitume): Inamifani mbili:

a) Tangu mwanzo kulikuwa mustari wa neema ya Mungu. Tunafata hile mustati tangu wakati wa Mitume, bila kuipasuka.

b) Kwa sababu Kanisa yetu inajengwa juu ya fundisho za wa Mitume wahubiri.

Kanisa letu haina umoja ya watu bore, lakini ni mwili wa Yesu Kristu unakaa ndani mwetu na Roho Mtakatifu. (Matayo 28,20. Yoano 14, 15017).

Kisha kufa kwa Mitume wa Kristu, wanafunzi wao wanakutana na ma askofu juu ya kuzungumuza mambo ya Kanisa namna yafaa kutembea Kanisa.

### SHINA LA HAKI YA KANUNI

Yesu Kristu yeye alilete mapenzi yake katika Mitume wake tunaipata katika Biblia Takatifu na Mapokeo.

-Biblia na Matoleo ya Mitume.

Shuruli (Jambo) ya mstari wa Kanuni iko ndani ya Agano Jipya, kwani katika Kitabu mwiko amri ya bwana Yesu kristu. kwa mfano: Amri ya Ubatizo, fazila ya Mitume, masikilizano ya Waaminifu wao...

-Katika Agano la Kale muna amri kumi ya mafundisho ile Bwana Yesu alitimiza katika Agano Jipya.

Matoleo ya Mitume ni nini? Ni fundisho ya Kanuni ya Kristu na Mitume wake, fundisho hii inaendelea kizazi kwa kizazi. Fundisho hii tunaipata katika mtaguso mkubwa, na vitabu vitakaitfu vya Mapdri wa Kanisa letu.

-Kazi ya Matoleo: Ni kutimiza kweli na kufafanusha Biblia Takatifu. Mtakaitfu Paulo katika kitabu ya Wathesalonika 15,6 anasema hivi: «Musimame muzuri muchunge matoleo muliyofundishwa sauti yangu. 1 wa Korinto 11,2) Hapa wanatuonyesha sawa vile walitupatia Matoleo ile tunapashwa kuichunga.

## KANUNI TAKATIFU

Kanisa yetu inatwelezea Kanuni gani iko ya kweli, na Kanuni hii inatupatia mapenzi ya Mungu.

Mutaguso (Makutano) wa kwanza wa muji Nikea wa njimbo ya Konstantinopoli ni yeye alifanya shauri. Mtakatifu Konstastinos Mfalme katika mwaka 325, kisha uzalio ya Kristu. Juu ya nini? Sababu ya kuhukumu mafundisho ya padri Arios; huyu alikataa Yesu Kristu kuwa Mungu; Yeye alisema ya kama Kristu alikuw akiumbe. Mutaguso hii ilileta Kanuni makumi mbili.

Mutaguso wa mbili wa muji Konstantinopoli kwa mfalme Theodosios mu mwaka 381, kisha kugombana na wa Heretiques (Ma kundi ya wakristu na fundisho wa uwongo) kwa wale waliomtukana Roho Mtakatifu. Watu walikataa Roho kuwa Mungu, wao wanasema ya kama ni moja nguvu. Hii Mutaguso alifanya ma Kanusi saba.

Mutaguso wa tatu mu muji Efeso mu mwaka 431, kisha mfalme Theodosios wa mbili juu ya kuhukumu fundisho ya askofu Nestorios. Huyu alikataa ya kama Mama Mzazi-Mungu alizaa Mungu, lakini alizaa paka mutu kwa hivi haiko vizuri kumuita Theotokos (Mzazi-Mungu) lakini Kristotokos, ni kusema Mzazi-Kristu. Ni kusema alizaa peke yake Kristu, alikataa hali ya kimungu yake. Aliandika ma Kanuni munane (8).

Mutaguso wa inne mu mwaka 451, kisha wakati wa mfalme Markianos, juu ya kugombana na fundisho ya Heretique ya wale walikataa hali ya pili, ni kusema hali yake ya kimutu. Hali ya mtu iliingia ndani ya hali kimungu ya Yesu Kristu. Vile ,wale wanafata hii fundisho ya uwongo wanaamini ya kama Yesu Kristu alikuwa paka na hali moja, hali kimungu. Lakini hii ni kosa mnane, kwa sababu Yesu Kristu aliishi na ma hali wa wili: Hali kimungu na kimtu, bila uchanisho, bila kuchanga, bila uharibifu katikati yao. Hii Makutano aliandika ma Kanuni makumi tatu (30).

Mutaguso wa tano ilifanyika mu mwaka 553 hile wakati ya mfalme ya Konstantinopoli Yustianianos juu ya kuhukumu fundisho ya asili.

Mutaguso ya sita mu mwaka 680 mu mji Konstantinopoli kwa nyakati ya mfalme Konstantino. Pale wa askofu walizungumuza juu ya kawaida ya dini.

Mutagusi wa Penthekti mu mwaka 696 hile wakati ya mfalme Yulianos. Mutaguso huu unafwata kazi ya mtaguso wa Sita na alitimiza kazi ya Mutaguso wa tano. Aliandika ma kanuni miya moja na mbili (102).

Mutaguso wa saba mu muji Nikea, wakati ya mfalme Konstantino wa sita na mama yake Irini, mu mwaka 787 ya hukumu wale waaminifu na wale wa askofu walikataa kubusu na kuheshimiwa ma Picha (Ikone) ya Bwana Yesu Kristu, Mzazi mwake na Watakatifu wote.

Kuna makutano ingine ya mkusanyo tuna ma Kanuni 85 ya Mitume ya Kristu.

Mu mwaka 251 tuko na makutano ya muji Khalkidona.

Mu muji Agira ku mwaka 314.

Mu muji Neokesaria ya Kapadokia ku mwaka 314. Waliandika ma kanuni 25.

Mu muji Gangra ya njimbo Paflagonia ku mwaka 340, waliandika ma kanuni 15.

Mu muji Antiokhia ya Siria, ku mwaka 341 waliandika ma Kanuni 21.

Mu muji Sardiki ya inchi Bulgaria ku mwaka 343. wal;iandika ma Kanuni 25.

Mu mji Laodikia ya Frigia, ku mwaka 381. Waliandika ma Kanuni 21.

mu mji Konstantinop0oli ku mwaka 394. Wa;iandika ma kanuni 60.

Mu mji Karthageni ya Livihi ya Afrika. Waliandika ma Kanuni 12.

Kanisa yetu inapokea ma Kanuni ile wapadri wetu walitumia watu wengine, hapana kwa wote, alichagua fundisho mzuri.

Ile Kanisa haina fundisho ya Bwana Yesu kristu inafaa kufwata 100% paka wa askofu wenye kutazama kabisa kabisa ile mambo, na mapadri wa roho kama tunafanya kiasi (ekonomie). Kanisa yetu inaleta uhuru wa roho na ma askofu wataangalia kama ni lazima kufuata ao hapana. Kanisa yetu inakataa kugeuza fundisho ya kawaida ya dini (Dogme) ni maongezo ao kugeuza katika kiasi, lakini kutii 100% . Kwani ma kanuni iliandikwa kufuatana na mambo ya kila wakati. Mapadri wa roho na ma askofu wanafanya kiasi, katika neema ya Mungu, wanafanya na mapendo juu ya kusaidia mtu ache kupoteza wokovu wake.

Kanuni ina wokovu kufuatana na ile wakati wa Mtaguso inafwatana na wakati. Mfano: Kanisa ilipata mambo ama hatari...Watu waliwaza kupita, waliandika, hapa sasa hawajui kitu.

# SURA WA KWANZA

## Kuingia ndani ya kanisa

1. 1 Katekismu na Msimamizi (Parrain).

Juu ya kuokolewa yafaa kuingia mu Kanisa na kupata ubatizo.

Bwana Yesu Kristu aliwapatia wa Mitume wake amri juu ya kubatiza yule anamwamini kwa Jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu (Matayo 28,19). Kama mtu haiingie ndani ya maji hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu (Yoano 3,5). Yule anasadiki na kubatiziwa, ataokolewa (Marko 16,16). Asili ya ubatizo:

-Imani kwa mukristu mwanzo ya Kanisa Katekismu ilifanya karibu miaka tatu (3). Hii miaka tatu karibu inafuatana na mambo ya yule mutu mwenye mapendo mingi na imani ya mtu mwenye kubatizwa kwa mwaka moja ao mbili (2).

Mwanzo wa karne ya tatu (milele wa tatu) ubatizo wa watoto uliingia pole-pole mu Kanisa «hapana mble ya ma siku makumi ine (40), lakini kisha ma siku makumi inne kwa watoto waliisha kukomea, fundisho ya Katekismu inafanyika kwa Msimamizi (parrain) wake. Lakini ni lazima kusaidia wwazazi wake na padri wa Kanisa.

Msimamizi anatajwa ya kama atafundisha mtoto yule alisimama kwa imani ya Kristu, kwa hivi yeye anasema Symbolo ya Imani na kusema unaacha shetani? Yeye atajibu pa fasi ya mtoto, mbele ya Mungu anataja.

-Msimamizi hawezi kuwa mtu wa dini ingine ao watu wa Kanisa ingine, wale wanalipizwa ku Kanisa. Mutawa hawezi kuwa Msimamizi, wazimu na watu wenye kuwa na mabaya; mzazi wa mtoto hapana.

-Kati ya Msimamizi na mtoto wa kubatizwa anaanza na mapatano ya kiroho. Msimamizi hawezi kufwanya ndoa na yule mtoto ao kuowa mama ya mtoto, wabinti na vijana hawezi kuowana kwani wana mapatano ya roho.

-Msimamizi hawezi kusimamia Nafsi mbili kwa kuepuka ndoa.

-Msimamizi wa kweli anabeba mtoto katika mikono yake.

Kanisa iko na namna ya kuweza kubatizwa mtoto bila Msimamizi wakati wa ugomvi.

1.2 Fumbo ya Ubatizo inaanza mu Katekismu juu yeye kukataa shetani na kazi yake (exorcisme). Kisha ibada ya katekismu inaanza ibada ya ubatizo. Fumbo ya ubatizo ni ya kwanza mbele ya ma fumbo ingine, ni mlango wa ufalme wa Mungu.

-Asili (Condition) juu ya kufanya ibada ya ubatizo bila kosa ni:

1) Yule atabatizwa (askofu ao padri) yafaa kuwa na upadirisho wa kweli (ni kusema kufuata Kanisa Orthodoxe) hapana kanisa ingine.
2) Haipashwe kufuata Kanisa ya uwongo ao mfariki wa shirika (Schismatique).
3) Yafaa kufuata mustari wa Mitume ni kusema kama anafuata Mitume ni kweli.
4) Yafaa kufanya upadirisho (ordination) ya kweli (yule padri ao askofu). Kama padri akifungwa na askofu hapashwe kufanya Fumbo ya Kanisa.

Kama Padri moja eko na zambi yake, bila kufanya maungamo ya kweli hana na neema ya Mungu, kwani ni mambo ya kweli.

5) Inapashwa padri kuwa na baraka ya askofu mbele ya kufanya Fumbo ya Kanisa. Kwa mfano: padri wa Kolwezi hawezi kwenda kufanya Liturgia ku mukini Lwalamba, bila ruhusa ya padri wa Parokia Lwalamba.
6) Padri anapashwa kufanya Fumbo na akili (mapendo) yake na kufamia nini anafanya.

## 1.3. FASI YA KUFANYISHIA UBATIZO

Kanisa iko pahali pote, katika mutoni, Kisanga na nyumba ya watu kama weko wagonjwa, lakini haina Kanuni: Ni paka mu Kanisa.

-Ubatizo unafanyika ndani ya maji mule tunaweka mafuta takatifu. Ubatizo wa kweli, kama tunamshusha mara tatu ndani ya maji ni kusema kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu. Kwani neno ubatizo ni kusema ndani ya maji.

-Hii mara tatu ndani ya kombe la ubatizo ni kusema Bwana Yesu Kristu alikaa ndani ya kaburi siku tatu kisha alifufuka. Iko sawa mtu wa zamani anaacha mambo ya zamani anakuwa mpya.

## 1.4. UBATIZO YA MU PEPO

Kanisa yetu inapokea ubatizo huu kama hatari iko mbele. Kama mtu eko mu hatari ya kufa, kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu. Ni namna padri, shemasi (diacre) ao mwaaminifu moja kufanya kama ni mu Orthodoksi. Yule anamubatiza anakuwa sawa padri hapana sawa Msimamizi. Kama ni huyu anabatiziwa asikufe tena, padri atafanya ibada Takatifu ya Ubatizo muzima.

-Kama padri akiuwa mtoto ndani ya maji wakati wa ubatizo yake askofu atamupatia kanuni ya malipizo (punition).

## 1.5.UBATIZO YA DAMU

Kama katikumeno moja mbele ya ubatizo wanamubamba kwiko adui na wanamupiga na anakufa, yeye anapata ubatizo ndani ya damu yake. Kwa ajili ya mambo ya Mungu. Eapagano wengine wanaona juhudi (courage) ya waamnifu wakati wa kufa, nao wanaamini na kufa, nao ni Washahidi.

-Mtu wakati ya ubatizo anabeba jina ya Watakatifu wetu, juu ya kufuata mifano yao. Lakini habebe jina ya audi wa kanisa, mwenye kutenda maovu (criminel) mpagano...

-Padri akiisha kufanya ubatizo ataandika watu ndani ya karatasi juu ya kuwapatia karatasi ya ubatizo (Certificat de Bapteme) juu ya watu kujua ya kama:

1) mtu huyu alibatizwa;
2) 2) Tena ni memba (membre) wa Kanisa Orthodoke.

-Jina ile atabeba mtu hawezi kuigeuza paka kama atakuwa mutawa. Padri mkubwa yake anaweza kuigeuza kwani anaanza uzima wa watawa, uzima mupya.

## 1.6. MATUNDA YA UBATIZO

1). Mtu kisha ubatizo anaacha ma kosa ya siri na zambi ile tulifanya wakati tunabatiziwa inatoka, ama inaondolewa.

2) Mtu wakati anabatiziwa makosa yake inasafishiwa na roho yake inabaki safi na zambi zote alitende tangu utoto hata sasa. Mtu alibatiziwa mbele, lakini yeye anafanya usharati kisha ubatizo eko na namna ya kupata upadirisho? Kwa sababu ubatizo ni kutakasa zambi zote.

3) Mtu akibatiziwa anabeba Roho Mtakatifu juu asifanya zambi ingine.

4) Mtu akibatiziwa ndani ya mwili wake munaingia kanisa ya Kristu na anaungana na Kristu; wa Orthodoksi weko wa jamaa moja.

5) Mtu akibatiziwa hawezi kubatiziwa tena mara ingine. Kwa mfano: Mkristu moja akivaa nguo ya ki padri na anasoma Misa, mafumbo zake ni ya uwongo kwani hakubarikiwa kwa Arkiaskofu.

-Mtu akipata ubatizo kwa padri wa uwongo anapashwa kwenda kwa Padri wa kweli kupata ubatizo wa kweli.

6). Memba moja wa Kanisa akikana imani ya Kristu akirudi mu Kanisa na kutubu, yeye hawezi kubatiziwa tena, lakini watamufanya paka krisma.

7) Mtoto moja yatima (orphelin), mwenye kuokota anaweza kubatiziwa kwani hatujui kama alibatiziwa ao hapana. Na ubatizo ni njia ya kwenda paradizo.

Kama mama eko mimba hatabatiziwa, si vizuri kusema na mtoto anabatiziwa. Mtoto mchanga akizaliwa inafai kubatiza.

## 2.MAFUMBO YA KRISMA

-Kisha ubatizo Fumbo ya Krisma inaendelea. Hii iko sawa muhuri (chapa) kwa yule mtu alibatiziwa.

-Fumbo hii inasaidia mtu katika uzima wake wa kiroho. katika Fumbo hii wale wenye kubatiziwa wanapokea zawadi ya Roho Mtakaitfu. Krisma ina na harufu makumi ine (40), ile inatuonyesha zawadi ya Roho Mtakaitfu ni nyingi wakati ya wa Mitume zawadi hii iliofanbyika ku mikono ya Mitume; kisha lufu yao. Kanisa yetu inaanza kutumia Fumbo ya Krisma. Sala ya krisma inafanyika ku kila Patriarkat mu kazi Ine Mkubwa ya Juma Takatifu na arkiaskofu huyu anapokea Mafuta Takatifu ku patriarkat katika mapendo na utii na heshima.

-Fumbo hii inafanyika paka kwa mapadri ao askofu wa Kanisa Orthodoksi, mbele ya kwanza Padri anaanza sala.

Padri yule atafanya Krisma atafanya alama ya Msalaba kisha atasema: Alama ya zawadi ya Roho Mtakatifu. Amina. Hakuna kiasi (economie) juu ya kufanya hile Fumbo ni paka kwa padri, mtawa ao mwaminifu.

-Kama mtu mmoja  anabatiziwa Kanisa ingine ya Kristu inafai kumubatiza katika Kanisa Orthodoksi na atapokea Fumbo ya Krisma ya kiasi.

-Mara ingine Kanisa inaweza kufanya kiasi kwa kupokea wale walibatiziwa mu Kanisa Romeo-katholiki na kufanya paka Krisma; hii iko paka kiasi.

-Wafariki wa Kanisa Orthodoksi weko na mambo paka ya matengeneo ya mwili, Kanisa inapokea mtu ule anatoka ndani ya kanisa ya wafariki inafai ku mupokelea na kusema neno anaacha kanisa na anarudi mu Kanisa ya kweli.

-Mwenye kusadiki hali moja ya Bwana Yesu Kristu inafaa kuwapokelea na kwandika neno na ku mufanya Krisma.

-Kama Mukristu moja wa Kanisa Romeo-katholiki anataka kufuata Kanisa Orthodokse ataandika barua na kusema ninaacha kanisa ya Romeo-katholiki na fundisho yakeya uwongo na fuata kanisa Orthodokse. Kisha padri atafanya Krisma, hii kiasi ni paka inchi wa Europe. Lakini kama huyu mwaminifu anataka kubatiziwa, itakuwa muzuri kabisa.

-Mukristu moja wa Anglikane anapashwa kubatiziwa kama anataka kuingia katika Kanisa Orthodokse. Hakuna kiasi mbele ya kanisa Anglikane.

-Vile inapashwa kufanya na wakristu wote wenye wanafata ma Kundi ya wa Protestantes. Wanapashwa kubatiziwa.

## MATUNDA YA MTU HULE ANAINGIA MU KANISA ORTHODOKSI

1.Mtu yule anaweza kwa kupokea Fumbo yote ya Eklezya yetu.

2. Yeye anaweza kutumika sawa memba wa Eklezya, sawa askofu, padri, shemasi, mutawa na ingine...na tena anaweza kutumika uzimamizi wa Eklezya.

3. Anapashwa kutii amri ya Kristu na shauri ya wa padri wa Eklezya.

4. Mtu yule anapashwa kuonyesha imani yake mbele ya Mungu na kwa watu wote wamuona sawa Missionnaire (mutume).

5. Mtu yule anapashwa tena kufuata Kanuni ya Eklezya yetu, sawa Liturgia Takatifu na ma sala ya Kanisa yetu yote...

6. Mtu yule anapashwa kusaidia na feza yake ku membo yote ile Eklezya atakuwa nayo na vilevile kusaidia maskini na hii vitu ni lazima mu kanisa ya parokia yake.

7. Mtu yule anapashwa kuwaza ya kama Kristu eko karibu naye kila siku na usiku mpaka mwisho ya uzima yake.

8. Ubatizo haienee kuongeza imani yetu, bila kufanya sala rohoni mwetu, lakini inafai tena kuungama.

## 3. KUUNGAMA (CONFESSION)

-Memba wa Eklezya juu ya kupata faida ndani ya roho yake, inapashwa ku kungombana na shetani, lakini atapata shaka rohoni, halafu Bwana Yesu Kristu hataacha yule mtu kumukombanisha, lakini atamusaidia kuungama sababu ya kumuondoa zambi zake.

-Uwezo wa kusafisha zambi unatoka kwa Bwana Yesu Kristu wakati aliwaelezea: (Matayo 18,18 na Yoano 20,23).

-Uwezo wa kuungama ulibebewa na askofu kwa Mitume wa Bwana Yesu Kristu, kisha wanawapatia Wapadri.

-Padri moja hawezi kuungama ama kufanya Maungamo bila ku mufanyia sala kwa askofu wake. Lakini ni mgonjwa mbele ya mwaaminifu wake ao kama yeye eko na lazima kufanya maungamo atamuonyesha askofu wake.

-Fumbo ya kuungama inafanyika paka na askofu ao padri hapana kwa shemasi, mutawa ao mwaminifu.

-Kwa kuungama ama kufanya maungamo inafai:

1).Ukweli na toba (ni kusema kuitikia kosa lake).

2)Kusema zambi zako katika mapenzi yako (usijishurtishe kwenda kuungama).

3)Muungamizi na mtoto wake wa roho wawe wa Ortrhodoksi.

4)Wakati Muungamizi anaungamisha ama anafanyishisha maungamo inamufaa kuvaa Epiotrahili, kisha kuungama Padri anapashwa kuweka Epitrahili yake huu ya kichwa ya mtoto wake wa roho na kumusomea sala ya maondoleo.

5). Kama padri wa roho hawezi kujibu mambo moja hivi ya nguvu kwa mtoto wake wa roho anapashwa kusimamisha kuungama na atamuuliza askofu ao padri mwingine wa roho. Atamuonyesha paka vile askofu atamujibu. Kama askofu anauliza atasema jina.

6). Tangu mwanzo mpaka wa milele (karne) wa ine maungamo ulifanyika mbele ya watu wengine, kisha milele wa inne ulifanyika kwa siri (mystique) sababu watu wasifahamu zambi ya wengine. Hakuna namna mtu kuungama mbele ya ma Ikone ya Bwana Yesu Kristu, hasemi hivi.

-Muungamizi naye anaungama kwa padri yake wa roho.

7) Pa kwanza kuungama inapashwa kuwa na umri wa miaka saba na ufahamu wakutumika na kujua mambo mema na mabaya.

## MATUNDA YA KUUNGAMA

1. Mtu anaungama anapokea zawadi na anaondolewa zambi na kosa zake zote.
2. Kwa hii Fumbo anapokea bunduki juu asitende tena zambi ingine.
3. Mtu yule anaungama anapashwa kusikilizana na Muungamizi mwake wakati gani kundi itafanyika kwake.
4. Muungamizi hawezi kusema mambo ile mtu anaungama; hata mbele ya uhaki (justice) kama Muungamizi anasema atahukumiwa na askofu wake.
5. Padri wa roho anapashwa kuleta malipizi ya umwalimu. Kwa mfano kusoma sala mingi, kufanya kwarezima (careme), ao kufanya kwa kupika magoti mara filani...ao bila kupokea Komonyo Takatifu.
6. Padri mwingine wa roho hawezi ku punguza malipizi ya mukristu moja yule anaitwa mtoto wake wa roho ao ubadilisho (mutation) ao musafari, ni namna askofu ao padri kushusha ama kutengeneza malipizi ya yule mtu aliungama.
7. Mtu yule aliungama kama ni karibu kufam, na malipizi yake ni mwake moja, padri wa roho atamuhurumia na atamupatia Komonyo Takatifu. Kama yule mtu anaishi malipizi yake itaendelea.
8. Kama, kwa mfano mwaminifu moja ni karibu kufa na hakuna padri ya roho karibu yake kusudi amuungame na huyu mwaaminfi anataka kuungama. atafanya nini? Kanisa Orthodokse inafanya kiasi moja. Nikusema huyu mtu ni karibu kufa ataungama mbele ya mwaaminifu muzuri zambi zake na kisha huyu atasema hii ma kosa na zambi yake kwa padri ya roho, hile wakati atamukuta. Padri ya roho atasoma sala ya usamehe yulu ya kaburi ya hule mufu, mwenye aliisha kufa.

## MAMBO YA MALIPIZI

Watu wengi wanakataa kuungama sababu ya malipizi ya padri wake muungamizi aliyomupatia. lakini malipizi ile haipatane na Fumbo ya maungamo.

-Watheologi ya Kanisa Romeo-Katholiki wanasema Fumbo ya kuungama haienee juu ya kutosha na kuondoa zambi. Inafai tena malipizi juu ya kutosha kasirani ya Mungu. Lakini si kweli, kwani Kristu alisulubiwa kwa mapendo ya Mungu. Lakini ya zambi zetu ni kule alitupatia Fumbo ya kuungama, Bwana Yesu Kristu si mtu mbaya, lakini yeye ni mwenye mapendo ana

lazima ya kuongeza malipizi sababu ya kumufurahisha Mungu. Tabia ya malipizi ni kukuponyesha hayuko ya kukulipiza. Tena malipizi inasaidia mtu uzito wa zambi yake; na kusopoka sababu asitenda tena zambi.

-Wakati wa malipizi kama mtu anatubu kweli, padri wa roho ataweza ku mushushia miaka, pahali pa mwaka moja itakuwa miezi munana.

## FUMBO YA EFKELEO (MAFUTA TAKATIFU)

Kisha Fumbo ya Kuungama kuna ingine inatuponyesha uzuri wa roho ni Fumboi hii ya Bwana Yesu Kristu alitupatia kufuatana na Evangelio ya Marko (6,7-13). Kule Marko anasema Bwana Yesu Kristu anawapatia Mitume juu ya kuhubiri na kupakaa wagonjwa Mafuta Takatgifu juu ya kuwaponyesha. Tena tunapata hii neno katika Barua ya Mtume Yakobo (5, 14). Kule anasema kama mtu ni mgonjwa inafaa kuwaita mapadri kuja juu ya kumuombea na kumupakaa Mafuta katika jina la Bwana.

Sala hii itamuponyesha na kuondoa zambi zake. Fumbo hii inatupatia zawadi mbili: Kuponyesha magonjwa ya mwili na usamehe wa zambi zetu.

Juu ya kutimiza hali ya Fumbo hii inafaa kuwa na vyombo ya kufanya nayo hii Fumbo:

1) Mafuta bila kuchanga na Manukato;

2) Fumbo hii inafanywa na mapadri saba, ao tatu ao mbili, tena kwa padri moja, kama hakuna mwingi.

Shina (Source): Katika Agano Jipya, Bwana Yesu Kristu aliwagawanya Mitume wawili sababu ya kutumika kazi yake sawa vile Mtume marko anatuwaambia.

3) Vile Mtakatifu Yakobo anasema kama kuna mgonjwa moja aite padri moja ao wengi.

4) Katika Eklezya Orthodoksi, kuna namna ya kufanya Mafumbo hii kwa mukristu moja katika muda murefu, kama mukristu ni mugonjwa saa zote. Fumbo hii inafanyika katika Eklezya kila mwaka mu Kazi ine Mkubwa ao tena katika siku mbili mbele ya kuzaliwa Bwana Yesu Kristu.

5) Padri anapakaa na Mafuta na kufanya alama ya Msalaba kichwani mwa wagonjwa kwa msalaba, chini, mulichafu, ndani ya kila mukono; yulu ya mukono na kisha mpakaliwa atabusu mukono wa padri.

N.B. Kama kuna mgonjwa moja, padri atapakaa pa fasi penye kumuumiza. Mafuta jii itabebewa na kupelekwa katika Eklezya ingine kama hayuku kwa sababu ya kupakaa waaminifu wengine.

6). Fumbo hii inafanyikwa pahali popote, ndani ya nyumba, mshamba na ndani ya Eklezya... Padri anapakaa paka Waorthodoksi na hapana wasio waorthodoksi ao hapana na wakatikumeno, kwa sababu bado kubatiziwa.

## FUMBO YA KOMUNYO TAKATIFU

Hali ya roho kuwa na faida ndani ya Eklezya ku kupokea Kommonyo Takatifu. Yule anakomunyika anaungama na Bwana yesu Kristu, kwani Yesu anasema; «Yule atakayekula Mwili wangu na mwenye kunywa Damu yangu mimi nitakaa ndani yake naye ndanio yangu» (Yoano 6,56).

Komonyo Takatifu ni Fumbo ya Mafumbo. Fumbo hii inafwanywa na askofu wakati wa kwanza na kunapashwa kuwa musaidizi. Kwa sababu katika askofu tunaona maungamo ya Kanisa kuwa fasi moja.

Askofu ni kicwa ya Kanisa naye ana fasi ya Kristu sawa kichwa ya kanisa. Ni lazima kabisa waaminifu kupokea Komonyo Takatifu. Kama haupokee Komunyo ya Mungu, malipizi yao itakuwa kadiri ya juma tatu bila kukomunyika. Hivi Kanuni ya Makutano ya Penthekti inasema: Huyu asiye komunika juma tatu, bila sababu anapashwa kulipizwa na Eklezya.

KIla mwaaminifu anapaswa kubaki ndani ya Eklezya mpaka mwishowa Liturgia kama eko tayari anapashwa kukomunika.

Wakati gani tunapashwa kukomunika?

Hayuko kanuni. Kwani Bwana Yesu anatuwaambia huyu atakula Mwili wangu,,,hapana paka mara moja, lakini bila kuacha. Juu ya kupokea Komunyo, kila wakati inafai kuomba baraka kwa padri wa roho. Huyu anakumunika bila kuacha ni vizuri juu ya uzima na wokovu yake.

hakuna mwaaminifu anaweza kukomunika yeye peke bila padri ao shemasi.

Kama mwaaminifu moja hakomunika, lakini anapokea Antidoro, pahali pa kupokea Komonyo. Tunapokea Antidoro pa fasi ya Komonyo, lakini bila faida munene, kwani antidoro haikombole Komonyo Takatifu.

Pa kupokea Komonyo Takatifu inafai kuwa na hali hii:

1) Kuwa memba wa Eklezya Orthodoksi. Hapana watu ya ma Kanisa ingine. Hakuna namna, kwani ni zambi munene.
2) Kuishi mu kanisa bila mafingo (malediction).
3) Kasma analipizwa kwa Muungamizi wake na tena ni karibu kufa, anapashi kukomunika. Lakini kama ataishi ataendelesha malipizi yake.
4) Yewye anayekomunika anapashwa kuwa na ufahamu wote. Kanuni wa 84 ya Makutano Penthekti inasema: Yeye anayepoteza ufahamu wake, hana na lazima ya kukomunika. Ila tu wa memba wa jamaa lake kama weko karibu kukomunika.
5) Kila mubatizwa mchanga ao mkubwa anaweza kukomunika bila kuuliza umri wa miaka.
6) Huyu anakomunika hatakuwa mtakatifu juu ya zambi ya mwili ao yeye anapenda kukomunika bila mapendeleo yake, hawezi kukomunika tena.

-Mwenye kufanya usharati (uzini) hawezi kukomunika, pa tapita wakati bila kukomunika (mpaka miezi tatu...) anaweza kuwa mtakatifu, nikusema mustahili ya kuishi katika sheria ya Mungu na kukombana shetani na ma zoezo zake mbaya katika neema ya Mungu juu ya wokovu na utakaso wake.

7) Kutakasa mwili haina kazi teke teke, lakini ni heshima mbele ya Fumbo hii.
8) Yule mwenye kuwa na kifafa anaweza kukomunika kama hana na hekalu.
9) Mwenye kupenda kukomunika anafunga bila maji ao chakula , katika kanuni 41 na 48 ya Makutano wa muji Karthageni. Ila tu wale wenye kuzimia wao wanapashi kupokea Komunyo Takatifu, pasipo kufunga ao mtoto mchanga pa kutafuta kuamuka anakunywa na anapashi kupokea Komunyo Takatifu, kwani haina kwa kutaka kwake.

## MIAKA TAKATIFU

Tangu mweanzo wa kuumba dunia Mungu alituchagulia siku ya saba sawa ya mapumziko. Hii sisi tunaungama siku ya saba na kupokea chakula cha roho.

Mkutano kati ya Mungu na mtu itafanyika kwa upekee ao kati ya watu wote.

Tuna kalenda tatu ya kanisa mule munapatikana vipande tatu ya sala ya Mungu ni:

1) Kundi ya kila siku.
2) Kundi ya kila juma;
3) Kundi ya kila mwaka.

a) Kufunga kwa kila siku ni: Sala ya kati ya usiku kisha ya asubui.

-Sala ya asubui, sala ya saa ya Kwanza, ya tatu ya Sita na ya Tisa. Sala ya Njioni (magaribi) na sala ya kisha chakula ya usiku (Apodipnon).

b) Sala ya Juma: Tunanyimbo mbele ya Paraklitiki, nyimbo yote ni katika Juma ya mnane. Juma ya kwanza tunaimba na sauti ya kwanza. Juma ya mbili tunaimba sauti ya mbili na hivi...Kisha ya Juma ya mnane tunafanya mara ingine paka ile nyimbo ya 1,2,3,4,5,6,7,8, nyimbo yote inaimbwa asubui na magaribi.

c) Kufunga kwa mwaka: Tuna Karamu kubwa ya Paska. Toka Paska inaanza Siku Kuu ingine. Kisha masiku Kuu ingine isiyogeuka, inaanza Siku Kuu ya Kuzaliwa kwa Bwana Yesu Kristu, na Kulala kwa Mzazi-Mungu na kwa Mitume Watakatifu na Watakatifu wa Eklezya yetu. Siku Kuu zingine hatufanye kazi, lakini siku zingine tunafanya kazi. Kwa mfano: Kuzaliwa kwa Bwana Yesu Kristu haipashi kutumika na siku Kuu ya Mtakatifu Theofilos tunatumika. Kama ni Mtakatifu Mkuu wa Eklezya hatufanye kazi, kwa mfano Siku Kuu ya Mt. Mushahidi Georgie.

## FUNDISHO YA KWAREZIMA

Katika kipindi Takatifu kuna ufafanushi moja ya kwarezima. Kwarezima inasaidia mtu kwa kufukuza zambi za mwili, kwani roho yake inanyanyuliwa kwenda mbinguni katika sala kwa kuona Utukufu ya Bwana Yesu Kristu. Kwarezima mbele ya Paska na mbele ya Kuzaliwa Kristu ni ma siku makumi inne.

1. Kwarezima inatwaambia Kanuni 69 ya Mitume. Kazi tatu na Kazi tano mkubwa wanafunga kanuni hii inasema kama askofu, padri, shemasi na shemaso mudogo wanakataa kufunga siku hizi. Inafai kuichunga hii nyakati ya Kwarezima. Paka kama mtu moja ni mgonjwa.

-Kama eko mukristu anakataa kufunga, Eklezya itamufunga.

Mitume walitupatia siku mu Kazi Tatu kwa sababu ya ukumbusho ile kazi kibaya alifanya Yudas ya kumutoa Bwana Yesu Kristu. Na mu Kazi Tano tunakumbuka usulubisho wa Bwana wetu Yesu Kristu.

-Katika siku hizi haipashi kula mayani, samaki, mafuta, jivini na nyama.

-Kila mposho na mu Juma tunakula mafuta ila tu mposho mkubwa.

-Eklezya inakatazwa kupadirisha wa Shemasi. Wa padri wakati wa Kwarezima ao kufanya (kuunga) ndoa. Kwani ni kipindi ya sikitiko na kutayarisha mioyo zetu sababu ya kujitakasa.

2) Kwarezima mbele ya Siku Kuu ya Kuzaliwa Kristu.

3) Kwarezima za Mitume

4) Kwarezima ya Kulala Mzazi-Mungu.

5) Kwarezima mu tarehe 5 ya mwezi ya Yanuaria, mu Siku Kuu ya Epiphanie na siku moja mbele ya tarehe 14 ya mwezi ya Tisa.. Ni Siku Kuu ya kupandisha Msalaba. Na tena mu tarehe ya 29 ya mwezi ya mnane ya kukata kichwa ya Mt. Yoani Mtangulizi.

6) Juma ya Diakenisimos, kisha Paska tunakula ma chakula yoyote kila siku, kwa sababu inaonekana kwa sisi sawa siku moja, siku ya Ufufuo ya Kristu.

7) Kisha Juma ya pentikosti tunakula vyote, sawa mu juma kisha Paska.

Kisha hii Juma tunaanza kwarezima ya Mitume Watakatifu mpaka siku Kuu yao, ni mu tarehe 29 mwezi ya sita.

## FUMBO YA NDOA

Fumbo hii haina wa lazima, lakini ni katika mapenzi ya kila mtu; lakini inasaidia watu kuishi muzuri na katika sheria ya Mungu.

-Ndoa mu Eklezia ni mfano wa kuungama sawa Yesu Kristu ni pamoja na Kanisa yake, hivi na watu wanaungana pamoja; vile anasema Mtume Paulo katika barua yake wa Efeso (5,22-33).

Ndoa ni masaidiano ya mume na muke kwa kutimiza kazi kufuatana na fazila ya Yesu Kristu.

Ndoa ni maungano kati ya mume na muke, kuwa na mwenendo moja ya uzima yao, mpashaji kanuni ya kimungu na ya kimutu. katika Fumbo ya ndoa Kanisa inabariki maungano na upashwa juu ya kuzaa watoto na kuwakomesha na kufika ku fazila ya yesu Kristu. Kwa sababu paka kwa hii jamaa ya Yesu Kristu ni namna kubeba watu wa ile fasi kwa ufalme wa Mungu.

Kwani jamaa iko sawa kanisa moja. Kwa hivi wazazi watafanya vyote juu watoto zao wakomee katika njia ya Bwana yesu Kristu.

hali juu ya kuunga Ndoa:

1) Watu wa wili wa hali ya kiume na kike (ama ya kuachana).

2) Kuwa na umri wa ukubwa mwanaume awe na miaka kumi na sita (16) mwanamuka karibu na miaka kumi na ine (14).

3) Wenye ndoa wajipende, padri anaombwe kwa waaminifu wajipende moja kwa mwingine na kuwaonyesha kwa kwingia katika Eklezya juu ya kushangilia ndoa ya Arusi.

4) Wenye ndoa wanapashwa kuwa na damu safi(njema) mara moja.

5) Ni lazima kujipimisha kwa mganga sababu ya kujua ginsi gani ya kuzaa watoto.

6) Mbele ya kushangilia ibada ya Ndoa wenye kuungana wanapashwa kumuona arkiaskofu. Huyu atawapatia kartasi ya ndoa. Wenye kuunga ndoa wataonyesha tendo moja (akte) na kusema ya bado kuowa bibi mwingine. Cheti (certifikat) cha uzima, baraka ya wa wazazi ao msimamizi wao kama weko chioni ya miaka kumi na munane.

Ruhusa ya wa akili wa utawalo wa wa polisi (Commissaire de police) kama ni laiki, kama tena ni askari anapashwa kuomba ruhusa kwa jemadari (general) ao wa Waakili (Comissaire) kama wenye kuunga ndoa ni wageni;

-Kama Bwana no Orthodoksi bibi ni protestanti, bwana atafanya tendo (acte) moja mbele ya wakubwa, na kusema watoto ni tazaa watabatizwa ku Eklezya Orthodoksi.

7) Yafaa kuandika tangazo mu Daftari (Journal)m radio ao mwaliko ya kusema tutaungana ndoa siku fulani na fazi fulani.

Kama Padri hatangaze atapata malipizi (punition).

8) Yafaa ma jamaa ngambo yote mbili kwa Bwana na kwa bibi kukubali, kama wazazi wanakataa ile ndoa, haitakuwa ya kweli. Fumbo ya ndoa inafanyika ku Kanisa ama ku parokia, kwa kiasi wanaweza kuunga ndoa katika nyumba yao. Wakati wa zamani Fumbo ya ndoa ilifanyika pamoja na ya Komunyo Takatifu. Sasa Fumbo ya ndoa wanaifanya namna kwachana. Wakati wa Kwarezima (Careme) hakuna kuunga ndoa ila tu kama kwiko shauri ya Eklezya, hapo tunaweza kuifanya.

-Padri yule ataunga ndoa wakati wa Kwarezima Fumbo yake ni ya haki, lakini arkiaskofu yake atasimamisha hule padri kwa muda kidogo.

-Fumbo ya ndoa inafanywa na padri kufwata desturi ya Eklezya Orthodoksi.

-Eklezya inakatazwa kuunga ndoa ku uficho.

-Padri ataandika katika kitabu chake cha Eklezya bila kizuio (obstacle).

## KIZIBIYO JUU YA KUUNGA NDOA

1. Upadirisho ni kusema, kisha upadirisho wa shemasi mdogo (Sous-Diacre) na kupanda juu hakuna kuunga ndoa kufatana na kanuni sita ya makutano Penthekti.
2. Uzima ya Utawa ni kukaa bila kuunga ndoa kisha kumunyowe kipara (tonsure) ya utawa. Ona Kanuni 16 ya matuguso wa 4 na 19 katika muji Agira ya Turkia.
3. Yule aliunga ndoa hawezi tena kuowelewa mara ingine.
4. Mwenye kuunga ndoa mara tatu hawezi tena kuunga ndoa mara ya inne ndani ya Eklezya Orthodoksi.
5. Kama wenye kupenda kuunga ndoa ni watoto si wakubwa.
6. Paka na ruhusa ya Serkali ao na baraka ya arkiaskofu.
7. Kama ni waviala ao wandugu na wa dada kuunga ndoa hapana.
8. Watoto wa baba, kambo moja ama wa kizazi moja wanakataziwa kuunga ndoa.
9. Mtoto wa muyomba anaweza kuowelewa na mtoto wa sangaji (ama muviala), kama baba anawowe bibi wa pili na huyu anazaa mtoto, huyu hawezi kuunga ndoa na watoto wa bibi wa kwanza.
10. Wandugu wa bibi yako hawezi kuwowana na dada zangu.

11. Bibi yako eko na mtoto ya dada yake, huyu akizaa mtoto mwingine na namna ya yeye kuwowa mtoto ya mtoto ya ndugu yake.
12. Watoto wetu wanaume wanapashi kujiowe.
13. Kama ndoa ikivunjwa usemeki unaendelea paka.
14. Usemeki wa roho unafanyika paka katika Fumbo ya ubatizo. Msimamizi hawezi kuwowa mtoto yule alisimamia awe binti wale kijana.
15. Kama Msimamizi akisimamia kijana ao binti hawezi kuwowana kwani wana padri moja wa roho.

-Mtoto wa kambo hawezi kuwowana na mtoto ya baba wa kambo ao ndugu zake wengine.

-Mlinzi hawezi kuunga ndoa na ndugu ya mtoto yule anachunga (kukomesha).

-Inakataziwa kwa mwenye kufanya usharati hastahili kuunga ndoa mume anaacha muke wake na muke anaacha mume wake hawataunga ndoa.

-Inakataziwa kuunga ndoa na watu wa dini ingine kwa mfano: Musulmano, wa Ebrania. Ila tu katholiki ao Protestanti. Fumbo hii ya ndoa inafanyika paka katika Eklezya Orthodoksi.

-Kama mama moja anavunja ndoa yake, anapenda kuunga ndoa ingine katika miezi mbili, tatu, ine Eklezya inamuonyersha kwa kuvumilia mpaka miezi kumi, kama inaunga ndoa Eklezya itaitika utaratibu (economie).

Kama bibi eko na mimba asichunge miezi kumi njo aunge ndoa, lakini inamupashwa kuunga ndoa mbele ya kuzaa.

Kama bwana ni askari inafaa kuomba ruhusa kwa wakubwa wake wa kazi. Lakini kama anaunga ndoa, mume anachukua muke wake na kwenda naye fasi ingine bila ruhusa ya jemadari. Eklezya ataitika Fumbo ile.

## MATUNDA YA NDOA

1.Umoja kati ya mume na muke katika roho na mwili, sababu ya kutimiza kazi ya kuzaa, kusihi katika roho bila kufanya usharati mpaka mwisho wa uzima wao, roho na mwili wanasaidiana sababu ya kukosa kutenda zambi.

2.Mume ni kichwa cha muke (Efeso 5,23). Ni mwongozi wa jamaa na mwenye daraka (responsable) katika mambo yote itakayofika.

3. Muke ni musaidizi wa mume kwa wakati wote na kwa mambo yote kisha bibi atapata jina ya pili ya bwana wake. kwa mfano: Isidora Katanga. Katanga ni jina ya pili ya bwana wake.
4. Wazazi juu ya kukomesha watoto wao vizuri sababu ya kufuata Eklezya Orthodoksi, wanapashi kutumika. Lakini watoto wabaki chini ya uwongozi ya baba zao. Kama huyu anafariki watabaki chini ya uwongozi wa mama zao. Ona kanuni (15 ya makutano ya Gagra.).
5. Watoto wanapashwa kuheshimu na kuwapenda wazazi wao wakati ya uzee, magonjwa ao wakati wa njaa. (Ona kanuni 16 ya makutano ya muji Gagra).
6. Ndoa haiwezi kuvunjwa ila tu kwa mapenzi ya Mungu. Baba na mama waungane mpaka mwisho wa uzima wao, lakini kwachana kwao paka kama kuna kitendo ya usharati, katika neno ya Bwana Yesu Kristu.

-Kama Mungu anaunganisha mume na muke hakuna mtu mwingine ataweza kuwachonganisha (Matayo 19,6).

-Kama askofu anasema ndoa haina ya kweli, inapashwa kumulipiza hule padri alifanyishisha ile ndoa.

-Kama muviala mwanaume wa kwanza anaunga ndoa bila padri kujuwa askofu akijuwa neno lile, yafaa kuliniza padri, na wale waliunga ndoa, kisha ile ndoa itavunjwa. Kama walizaa watoto ni wa haramu (batard) hawana wa kweli.

## TALAKA (DIVORCE )

-Kanisa (Eklezya) yetu inapokea Talaka moja ya kizalikio na lufu ya bwana ao bibi. Lakini kwa ajili ya utaratibu (economie) Eklezya yetu inapokea namna ingine ya kubomoa Fumbo ya ndoa.

-Juu ya nini Fumbo ya ndoa ni lazima katika ubikira?

1. Usharati (matayo 5,32).
2. Kuunga ndoa na bibi mwingine bila wa kwanza kujua ao bwana wa kwanza kujua. (Hapa inapashi kuomba buku ya kuachana (acte de divorce) ku Kanisa.
3. Bwana akipiga bibi yake katibu kufa ni lazima bibi yule kwachana na bwana hule. Ao bwana anaruhusu bibi yake kufanya ukahaba bila kutaka kwake, bibi eko na uwezo wa kwenda ku Kanisa kuomba ruhusa ya kuachana (divorce).
4. Kama mume anaacha bibi yake juu ya kutafuta bibi mwingine kisha miaka makumi mbili na moja (21) eko na uwezo wa kwenda ku Kanisa kuomba ruhusa ya talaka.
5. Kama bwana anashurtisha bibi yake kutosha mimba, lakini bibi anakataa, bibi eko na uwezo wa kwenda ku Kanisa kuomba ruhusa ya talaka.
6. Kama muke ao mume anataka kuwa na uzima ya utawa, inafaa kupata ruhusa ya wote na kupata hakikisho ya bibi yake.

## NAMNA INGINE YA TALAKA, PASIPO KOSA YA BWANA WALA YA BIBI

1. Kama bibi na bwana awazaa watoto ni namna kisha miaka tatu bibi kwacha bwana na kwenda kuolewa fasi ingine. Kwa hii neno paka kama bibi anapenda. Kwani haina kosa ya bibi ao ya bwana.
2. Kama bwana ao bibi kati yao moja eko na magumu. Kisha miaka ine ile ndoa iko na namna ya kuharibika.
3. Kama bwana ao bibi eko na magonjwa ya ukoma. Na namna bwana ao bibi kwachana. Lakini sasa magonjwa hii kuna namna ya kuiponya, haina namna ya kuharibu Fumbo ya ndoa ile.
4. Kama bwana amesha kwenda fasi fulani muda murefu, bila kusikilizana na bibi yake, bibi eko na uwezo wa kwenda kwa askofu juu ya kumuhukumu bwana katika neno lake. Kisha askofu ataenda kwa wakili (procureur) kumupashwa hii neno juu ya kumuhukumu. Kisha atakuwa na uwezo wa kuvunja ndoa.

## MATUNDA YA TALAKA

-Kama bibi anavunja ndoa, anarudi kwenda ku nyumba yao na anabeba jina la baba yake atakataa ya bwana yake.

Bwana wakimurudishia mali, eko na uhuru wa kuunga ndoa ya tatu, lakini bibi hana na uwezo wa kuunga ndoa mara tatu kama wanaachana na bwana yake.

-Kama kosa ni ya bwana ruhusa ya serkali bibi atabeba watoto. Kama watoto wangali wadogo na kosa iko ya bwana, bwana anaombwa kuleta feza, sababu ya kununua nayo chakula ya watoto wake.

-Kama kosa ni kwa wote bibi ao kwa bwana ndoa yao inavunjwa haina lazima bwana kuleta feza ya kununua chakula. Hapa bwana hana na ruhusa ya serkali, lakini akipenda atawasaidia watoto wake.

-Watoto wa ndoa ya kwanza wa watoto wa ndoa ya pili ni wa ndugu wa mwili.

-Kama ndoa inavunjika, lakini usemeki, umama muko unaendelea. Bibi na bwana wakipenda kurudishana, Kanisa hatawafanyishisha tena ndoa paka sala ya usamehe.

-Inakatazwa kuweka taji mara ya pili kwa mtu hule anakataa kuwowa bibi mwingine. Paka kumufanyishia Fumbo bure bila kumuvika taji. Kwani taji inaonyesha uzima ya ubikira.

# SURA WA TATU

## TAFAUTI KATI YA MWAAMINIFU NA MAPADRI

-Achanisho hii inasaidia matengeneo mzuri ya Kanisa. Vile Kanisa ni mwili ya Bwana Yesu Kristu na waaminifu ni memba ya hii Kanisa yake na kila memba wa Kanisa ni lazimi kusaidia mwili (Kanisa) (1 Wakorinto 1,12,14).

## KAZI YA WAAMINIFU

-Mbele ya mapdri wa kipimo ya chini, lakini wa laiki (waaminifu) wanatumika kazi ya utawala wa Kanisa. kazi hii inatoka ku uwezo tatu ya Bwana Yesu kristu, huyu alikuwa Kuhani mkubwa, Mfalme na Nabii. Kwa uwezo wa Bwana Yesu kila mwaaminifu anapokea wakati wa ubatizo na Krisma. (Ufunuo 5,9-10).

-Wa Laiki (waaminifu) wanasaidia padri ku sala; sawa watoto wanabeba phanari, (mishumaa ao taa), epitafio, weko waimbaji, memba ya kamiti (comite) wakusafisha Kanisa, wakufanya prosforo, watoto ndani ya Altari Takatifu. Laiki wanatumika na kusaidia padri ku kila siku kuu (fete) ku Liturgia.

-Wa Laiki wanasaidia mafundisho ya Eklezya kwa baraka ya askofu ao padri. Juu ya kuhubiri, katekismu. Eklezya ya zamani Katekismu ilifanyika paka na askofu ao kwa mwalimu moja yule alipata baraka ya askofu.

-Wa Laiki wanasaidia Utume (Mission ) kwa kazi mbalimbali sawa kutembelea wa maskini, kuleta saidio kwa watu wasiona namna, kugawanya vitabu, picha ya watakatifu na ingine...

-Kabisa kabisa waaminifu wanatumika katika utawala wa Kanisa. Kila Eklezya (kanisa) ina kamiti ya wa baba na wa mama wale wanaongozwa kwa utawalo wa Eklezya. Katibu (secretaire) juu ya kutengeneza cheti ya ubatizo, mlimbiko (resor), kitabu...Wakamiti wanaweza kuchagua mtu fulani kuwa padri wa Eklezya lao na kusema wakati ya upadirishoi anastahili, anastahili (Aksios, aksios).

-Waaminifu wanatumika kwa makutano sawa kufwata kanuni, mstari wa Kanisa (Eklezya) ulifanya na Laiki ao wa padri. Ni vile wa Patriache wa Eklezya Orthodoksi waliandika barua moja na mu le 6-5-1648. Juu ya kwenda fazi yote kule kunapatikana waaminifu Orthodoksi.

Barua ile iliandikwa hivi:

«Taifa ni mchungaji wa Orthodoksi. Waaminifu Orthodoksi ni mwili wa Kanisa. Lakini mwenye daraka ya matengeneo yote ni askofu. Ni huiyu anapashwa kufundisha Kristianisme ama kanuni (dogme_ na kuichunga».

-Waaminifu wanapashwa kutii mapadri na maaskofu katika mustari ya (WaEbrania 13, 17).

-Achanisho ingine kati ya Laiki na padri ni hali (sexe) ao kipimo. Kwa mfano: Mama moja hawezi kuingia ndani ya Altari Takatifu, kufundisha, kufanya metania, phenari ao kuvaa nguo sawa mtoto wa Altari Takatifu. Kazi ya mama ni kukaa mu Kanisa na unyenyekevu na kutii mbele ya padri (1 Timotheo 2,11 na 1 Petro 5,5).

## KAZI YA WATAWA NDANI YA KANISA

Kati wa laiki na mapadri ni kundi ya Watawa. Mutawa haina laiki ao padri. Wao wanatabia ya mapadri: Mfano hana manguo, lakini hawana cheo ya upadirisho na uwezo.

uzima ya utawa haina ya ugeni, lakini ni Bwana Yesu Kristu alileta wakati alishauria kijana moja mtajiri akisema: «Ukitaka kuwa kamilifu uzisha vitu vyako vyote na utapata mali ya roho juu mbinguni» (Matayo 19,21 na Matayo 19,12).

Hivi tunaona miaka ya kwanza waaminifu waliacha mali zao na kufunga (jeune) pale paka uzima wa ubikira ulianza. Tangu karne (siecle) ya tatu waaminifu wale walipenda kufuata utawa, walianza kuishi jangwani. Kila mtu anaishi peke wanamuita mutawa (moine).

Baba wa kwanza wa uzima wa utawa ni mt. mkubwa Antonio, huyu ni padri wa uzima wa Utawa.

Matengenezo ya uzima ya utawa ni hii:

1. Mweremiti.
2. 2. Uzima wa baba wa roho na karibu yake wanafunzi walijenga nyumba. Kila juma wanaenda ku kanisa kufanya Ibada ya Liturgia.
3. Mtawa anayeihsi katika ushirika anaishi sawa wa jamaa moja na baba wa roho na mtawala. Kila mutawa eko na chumba (chambre) chake. Kuna utaratibu, ao (maombi moja-moja, chakula moja, kila mtu eko na chumba chake cha maombi).

Tangu karne ya 14 mwanzo wa Monasteri ni kusema ndani ya Monasteri hii kila mutawa ana na mali yake na chakula chake katika chumba chake. Paka kama ni siku Kuu kubwa Watawa wote wanakuja pamoja. Monasteri ataleta makuta kidogo. Wanafanya sala yao pamoja ku Monasteri ndani ya Eklezya (asubui, kati ya muchana na magaribi).

Katika jimbo moja kuna Monasteri inatii ku Metropoliti pale muji Grekia (Crece) tuna Monasteri ya Patriarche wa mutaguso wa Konstantinopoli. Wnakumbuka patriarche kastika Liturgia. Wenye kuwa chini ya upatriache wana na monasteri inaitwa Patriarchat ao Stavropigiaka. Jina ya Stavropigiaka maana yake wakati wanajunga Eklezya wanafanya katikati yake na usingi yake alama ya Msalaba, mbele ya kufanya usingi (fondation).

## NAMNA YA KUPATA UZIMA YA UTAWA

Hakuna kizibio juu ya kufuata uzima ya utawa bila mambo ya kufuata hali, uwezo...Kila mtu anaweza kufuata uzima wa Utawa kwa sababu unaleta amani. Neno nzuri na ya kuachana ni hii:

1. Pa kimwacha bibi inapashwa na ruhusa ya serkali. Ao masikilizano na bibi (bwana) yake.
2. Anapashwa kuwa na umri wa miaka karibu makumi mbili na moja. Pa kuingia ku monasteri ya Mulima Takatifu ni kuwa umri karibu kumi na mnane (18) yafaa kuwa na afya njema yasiyo na magonjwa.
3. Kwa kuchagua uzima huu yafaa mtu kuwa uhuru (libre) bila kuwa na shaka, kukosa oga, kuleta nguvu kwa watu wengine.
4. Kama monasteri inajaa, yafaa kuchagua monasteri ingine.
5. Yafaa kupima uzima ya Utawa kadiri ya miaka tatu. Kuna wengine wanapenda kujiongezea miaka tatu ao kutosha miaka tatu, lakini hana na uwezo, mwenye kuwa na uwezo paka padri wa roho.

6. Wakati anapata cheo ya Utawa wanamusomea sala ya saa moja. Mutawa atalapa ya kama nakamata uzima ya ubikira. Ya umasikini inafaa kuwa na valise ndogo, maana yake yafaa kuchagua uzima wetu bila kutenda zambi.

7. Padri wa roho anakata nywele kwa alama ya msalaba; ni kusema akili yake inabaki mbale yeye atatii paka kwa padri wake wa roho. Sala ya Watawa ni ubatizo wa roho na Mungu anamusamehe zambi zake.

8. Sala ya utawa inafanywa na askofu ndani ya Mitropolia yake. Na Igumeno (padri mukubwa) anafanya kama anapewa haraka kwa askofu wake, na tena anapashwa kuwa arkimandritis.

9. Fazi ya kufanyia sala ya uzima ya utawa ni ku Monasteri kule ataishi miaka yote katika uzima wake.

## MATUNDA YA UZIMA YA UTAWA

1. Mutawa ni memba kweli wa Monasteri yake. Anawezi kutumika kwa utawala (administration) wa monasteri yake, anaweza kuwa padri, shemasi wa monasteri yake.

2. Mutawa katika dunia hii eko kama mufu kwani anatoa uzima wake katika kazi ya Mungu. uzima huu kwake ni mupya. Mutawa atapata jina mupya, nguo mupya mweushi na fazila tatu ya utawa sawa msingi. Ni: Utii, ubikira na umaskini.

3. Mutawa hawezi kurudi duniani kutenda kazi ya dunia kama politiki, usimamizi wa muji ao wa serkali.

4. Kama mutawa moja ni padri hawezi kufanya Fumbo ya ndoa paka na baraka ya askofu wake.

5. Mutawa hawezi kuwa msimamizi ku ubatizo wa mtu moja, ao hawezi kuwa mulinzi nikusema (baba yake akifa yeye hawezi kuleta wandugu wa jamaa yake).

6. Yeye hawezi kwenda inje ya monasteri bila baraka ya padri mkubwa yake.

7. Yeye hawezi kwenda monasteri ingine katima uzima wake bila baraka ya padri mkubwa yake; paka kama askofu anamuita juu ya kumupatia cheo ingine ao juu mambo ingine.

8. Uzima ya utawa ni sawa uzima wote hakuna namna kuacha, kwani ni malapo. Mutawa akiwowa hawezi kupokea Komonyo takatifu hata mara moja mu uzima yake, tena hawezi kuokolewa kwani ni mafingo ya Kanisa. Huyu mutawa laiyeacha monasteri yake na aliingia kuishi duniani ni mutoaji ya Kristu.

9. Sala ya utawa inafanyika paka kwa mara moja tu.

10. Utawa una daraja (vipande0 tatu ao mbili ni:

Mwanafunzi (novice( ni mwaka moja ao tatu kisha padri mkuu wa monastyeri atasoma sala mbili inaitwa rasoforia. Ni kusema navaa raso (manguo mweushi) na napata jina mupya na anamupatia mandia. Mweushi na kunyowe nywele kwa alama ya Msalaba. Kisha cheo hii kila miaka tatu kuna ibada ya Megaloskimo. Ni kusema mkubwa Alama wa utawa. Wanavaa inje nguo moja pa hile yake ni Msalaba mkubwa na inamuchunga mutawa moja sawa ukuta.

11. Mutawa hawezi kuunga ndoa.

12. Tena hawezi kuwa na mali mingi, magasini na ingine...Akiwa na mali mingi mbele ya kwingia ku Monasteri yafaa kugawanya ao kuacha ku monasteri, lakini akipenda kutoka hawezi kubeba ile mali yake.

13. Faida ya uzima ya utawa ni kuwa na roho ya uvumilivu mu Kanisa na mu jamaa. Kila monasteri ni kichwa cha majifunzo ya ufalme Orthodoksi wetu walikuwakako na wale weko.

14. Ufalme Orthodoksi unasaidia kazi ya Utume na ni sawa chombo moja cha kusimamisha zambi za dunia.

# SURA WA INNE

# KAZI YA MAPADRI

## FUMBO YA UPADIRISHO

Padri yeye eko juu ya Watawa, Mapadri wanaendelesha kazi ya Mitume. Fumbo ya upadirisho ni kupokea uwezo tatu ya Bwana Yesu Kristu, nikusema: Kuhani, Nabii na Mfalme. Hii ni uwezo wanapokea mapadri. katika uzima wao wanafanya Fumbo sawa Makuhani makubwa, sawa manabii ya Bwana Yesu Kristu na sawa Wafalme, kwani kazi yao ni ya kuzambaza habari njema duniani nzima.

Uwezo wa mapadri haina ku mapenzi yao, lakini ni roho ni kazi ya mapendo (2 Korintho 13,10) na kusema kila padri hana paka na uwezo wa kusaidia watu juu ya kujenga fazila ya roho zao.

Upadirisho ni Fumbo ya Kanisa. katika Fumbo hii wanapokea uwezo wa Bwana Yesu Kristu, kama askofu ananyosha mukono wake kichwani.

Kuna cheo tatu ya upadirisho: Shemasi. Presviteros (padri) na askofu.

Fumbo hii inafanyika katika Altari Takatifu. Paka ile wakati na Fumbo ya Komunyo takatifu inafanyika.

Upadirisho ya shemasi inafanyika mbele ya sala ya Baba yetu uliye mbinguni...

Ya padri inafanyika kisha Kuingia kubwa.

Ya askofu inafanyika kisha wimbo ya: «Mungu mutakatifu... na mbele ya somo ya Matendo ya Mitume (Apostolos). Juu ya nini? Juu ya kufanya Fumbo ya Komunyo Takatifu.

Tuna cheo ingine ndogo:

-Shemasi mudogo, msomaji, mwimbaji na neokoros (Ni huyu mutumishi anayefanya kazi ya Kanisa (kandili, mishumaa, ubani, usafisho na kazi ingine).

-Kwa kupata uwezo hii, askofu anawekea watu hawa mikono yake inje ya Altari Takatifu, na anasoma sala moja

Zamani kulikuwa cheo ya mwanamuke wanamuita Diakonisa, lakini hakwanza kufanya kazi ya shemasi mwanamuke, walianza kusaidia padri ku Fumbo ya ndoa kwa kusaidia wanawake. Kuvaa vizuri. Leo hii cheo inesha kumalizika.

Askofu anasoma sala kwa wa mama bikira ao msiye na ndoa kwa baraka ya askofu atakuwa na uwezo wa kwingia ndani ya Altari Takatifu.

## UWEZEKANO JUU YA KUFATA UPADIRISHO

1.Yafaa kuwa mbatizwa na Krisma ya kweli ni ndani ya kanisa Orthodokse.

2.Yafaa kuwa mwanaume hapana mwanamuke.

3.Shemasi yafaa kuwa na miaka makumi mbili na tano (25) na padri yafaa kuwa na miaka makumi tatu (30). Kanuni 14 ya Makutano Penthekti).

4.Yafaa yule mtu kuwa na imani ya Kiorthodoksi. Mfano katika miezi mbili kwa kupokea upadirisho.

5. Yule anakataa kuwa padri akitaka kwa shemasi inamfai kuchunga wakati juu ya kuwa padri. Tuna mfano; Askofu anaweza kufanya mu juma moja mtu kuwa shemasi ao padri, askofu patriarki (sawa mtakatifu mkubwa Fotios). Ila tu katika lazima, lakini haina uwezo wa Eklezya.

6. Yule mtu anapashwa kujuwa Biblia takaitfu na Kanuni ya Eklezya. Kule Grekia pa kuwa na cheo ya Uaskofu yafaa tena kuwa na cheti cha serkali cha dini ya Theologia zaidi chenye kuleta na Arkiaskofu. Kuwa shemasi ao padri inapashi kuwa na cheti cha masomo ya Theologia.

7. Yafaa kuwa mfwasi (bila kilema). kanuni za Mitume 18. Usiwe na magonjwa ya tumbo. (kanuni 22 za Mitume).

8. Mtu yule anafaa kuwa na akili na afya nejma bila kifwafwa (Epilepsie)ao na mashetani.

9. Yafaa kuwa muuhuru phapana kuwa mtumwa. Bila mambo ya kabila ao cheo. Ona Kanuni 82 za Mitume.

10. Wanapashwa kuwaweka heshima na sifa kwa watu wengine. Kushuhudia vizuri watu wengine. Kwani hawezi kufundisha watu wengine kuwa na mifano yake. Ona Kanuni 12 ya mutaguso ya muji Laodikia.

11. Kama tunasema yafaa kuwa na ushuhuda nzuri kwa watu wengine nikusema:

a) hapana kukataa imani ya Kristu ya zamani ao ya sasa.

b) Hapana kufanya kazi bila sifa. kwa mfano: Kama binti moja anatumika ku bara, lakini yeye anatenda usharati yeye analetea baba yake feza, huyu baba hawezi kuwa padri.

c) Yeye kama aliiba mali ya watu wengine.

d) Kama yeye anafanya biashara na anakusanya makuta mbaya, hawezi kuwa padri. Anaweza kuwa padri paka kama anatubu makosa yake na anafanya maungamo kwa padri ya roho yake.

e) Yeye akiapa kwa sauti ya uwongo hataweza kuwa padri.

f) Kama aliuwa mtu ku mapnezi yake ao bila mapenzi yake hasitaweza kuwa padri.

g) Akitenda usharati kisha ubatizo wake, hawezi kuwa padri. Vile kanuni ya mt. Basile mkuu inasema; kanuni 69.

h) Kama mutu yule anauza cheo yake kwa askofu, yeye hawezi kuwa padri.

i) Kama mtu yule alihukumiwa ku baraza kuu katika kitendo (kiasi fulani) Eklezya yetu inasema huyu mtu hawezi kuwa padri.

j) Kama mkubwa wa jamii ndoa yake haina na kosa, yeye hakuwowe semeki yake yafaa kuwowa mugeni.

k) Inapashi kuwowe mwanamuke moja, lakini kama akiwa na wanawake mbili hawezi kupata upadirisho.

l) Kabisa kabisa askofu yafaa kuishi bila ndoa. Ona Kanuni 12 ya Makutano Penthekti.

m) Kama bibi anawowelewa mara ya kwanza kisha anaunga ndoa mara ya pili bwana yake hawezi kuwa padri.

n) Msiye na ndoa ao mwenye kuvunja ndoa bwana yake hawezi kuwa padri.

o) Kama bibi yake alikuwa mtumwa ao msimamizi, bwana hawezi kuwa padri.

p) Yafaa bibi na watoto wote kuwa Waorthodoksi wasiwe na Kanisa ingine.

q) Kama mtu moja anapata cheo ya upadri, lakini yeye alikuwa na kosa kufwatana na maneno tunasema juu. kanisa itamupatia kanuni bila kufanya Fumbo hata moja.

r) Mtu anapashwa kupata cheo ya padri, shemasi ao askofu paka mara moja tu hapana mara mbili ao tatu.

s) Fumbo ya upadirisho yafaa kufanyika mbele ya watu wote juu ya kuonyesha kama wanamupenda nikusema anastahili anastahili (aksios, aksios).

t) Askofu mbele ya kupadirisha mtu yafaa kumupatia shemasi ao padri fasi yake.

u) Mutu hawezi kupata upadirisho wa shemasi-mdogo ao padri katika muda kidogo. Si vema ifanyika hivi (shemasi-mdogo, shemasi ao padri).

v) Si vizuri kuleta feza ao kwa wakubwa wa kiasi (politiki) sababu kuomba upadirisho wa mtu fulani.

w) Pa kupadirisha mtu inafaa yeye kupenda. Lakini kama unapokea cheo ya shemasi yafaa vilevile kuwa na cheo ya upadri.

x) Kama mtu anataka kuwa askofu, yafaa kuita Eklezya maaskofu tatu juu ya kumupadirisha. Lakini shemasi ao padri paka askofu yeye moja anawezi kumupadirisha.

## MATUNDA YA UPADIRISHO

Padri anaombwa kwenda pahali ile askofu anamuweka kisha upadirisho wake.

Kama askofu na padri wanasikilizana kupadirishana mara ya pili wote wa wili watawatenga katika shirika (excomunier). Kama askofu ni mtinina wa dini analeta kwa mtu fulani cheo ya upadri. Askofu yule si wa kweli, lakini wa kweli ni yule anafanya upadirisho wa kweli.

Padri mwenye kubeba Eklezya ni yule anabaki pahali pale. Kutumika paka askofu anamuruhusu kwenda ku Kanisa ao ku monasteri ingine.

Padri mmoja, shemasi ao askofu akiwafanya kosa fulani atabaki na cheo paka yake akuna namna kumushusha (degrader) kwani ni chapo (cachet).

Padri ao shemasi moja asitaacha kazi zake, kwani Fumbo ya upadirisho ni sawa stampa (cachet).

## KAZI YA LAZIMA YA KIPADRI

1. Kuomba bila kuacha na kusaidia pasipo kuchokesha roho ya waaminifu wake. Kwa sababu Mungu atamuhukumu. (Wa Ebrania 13,17).
2. Padri anapashwa kuchunga mwili wake safi bila kutenda zambi ya dunia (Kanuni 25 ya Mitume na 70 ya mt. Basile Mkuu)
3. Padri hana na uwezo wa kuunga ndoa kisha upadirisho wake.
4. Kama bibi ya padri akizini na mume mwingine, padri anapashwa kufukuza muke yake. Kama yeye anapenda bibi yake ataacha kazi ya upadirisho yake.
5. Juu ya watoto kuokolewa inafai kuwasaidia na mafundisho ya Bwana Yesu Kristu, hapana kwa watu wa Eklezya ingine.
6. Padri ao shemasi hakuna namna ya kusihi na muke mwingine paka na mama yake, dada yake, dada ya mama yake na semeki yake.
7. Padri anapashwa kuvaa nguo za kipadri ndani ya nyumba na inje ya nyumba yake. Kanuni 27 ya makutano Penthekti. Ndani ya nyumba yake hakuna namna kutosha kanzo mbele ya watoto wake, hawataleta heshima kwa baba yao.
8. Padri hana uwezo wa kufanya biashara(commerce( ao kupokea kodi (taxe) ao kufanya magazini.
9. Padri ao askofu hawezi kwingia ndani ya kiasi (politiki) ao tena kutamani cheo ya politiki. Askofu ao padri weko na uwezo wa kupokea cheo ya upresidenti kama taifa inamupenda na serkali yake mu utumwa.
10. Padri hawezi kwenda ku baraza kuu (parquet) juu ya kustaki watu wengine. Lakini wakati padri wanamuita wanamusikitisha, yeye atauliza askofu wake atafanya nini.
11. Si vizuri padri kupiga waaminifu ao wasiyo na imani (mapagano) kwa ajili ya mawazo yake juu ya kufanya elimu ya kufundisha. Si vema kustaki katika kanuni ya 27 ya Mitume.
12. Si vema kukopesha feza na faida katika kanuni 17 ya mutaguso wa Kwanza.
13. Si vizuri kuwa na mapendo ya feza ai kuiba vitu fulani, kutushi wakubwa wa serkali ao kusema maneno ya zambi ao kuwa wasema mingi, tusinawe pamoja na wanawake ao kuzunguka bila sababu.
14. Padri anapashi kuishi katika uzima safi na muke wake awe wa mifano mzuri mbele ya watu wengine.

## KANUNI YA MPADRI

1. Halasa (Salaire) yake ni Kanisa ama waaminifu ao mushauri ya Eklezya inalipa Padri.
2. Kama Serkjali iko mu ugomvi padri asikamata bunduki na kupiga, asivaa nguo sawa askri ao asiende ku baraza kuu, lakini masemo yake iwe ya haki na kweli.
3. Padri anapashi kuheshimiwa na waaminifu na wakubwa wa serkali na katika siku kuu.
4. Hakuna namna serkali katika usawa wake (ordre) kufanya kazi yasio haki mbele ya wapadri kwani mapadri ni watu watakatifu.

## MAPASHWA (DEVOIR) YA MAPADRI

1. Askofu anabeba mapashwa yote sawa vile yeye eko na uwezo wa Bwana Yesu Kristu, sawa kuhani, nabii na mfalme. Analeta ripote yake ku makutano kubwa wa Eklezya.
2. Mara moja padri ataanza mapashwa yake mu parokia na ataleta ripoti kwa askofu wake. Mapashwa ya padri ni pamoja na askofu. Lakini paka kwa kazi hii padri hawezi kufanya:

-Upadirisho.

-Hawezi kufanya sala ya kuweka mikono yulu ya shemasi-mudogo ao mwimbaji.

-Kusoma sala ya kutaryarisha Mafuta takatifu.

-Kufungula Eklezya mupya.

-Kusoma sala ya Antiminsion; kungama bila baraka ya askofu.

-Kusoma Ibada ya utawa (paka Igumeni (padri mkubwa)eko na ruhusa kufanya hii Ibada kwa Watawa wanaume na wanawake).

-Shemasi hawezi kufanya Fumbo hata moja kwa sababu yeye ni msaidizi wa askofu na padri.

## CHEO NA UWEZO WA EKLEZYA YA KRISTU

Katika Eklezya yetu tuna cheo tatu:

-Shemasi, padri na askofu. katika shemasi tuna shemasi-mkuu, nikusema shemasi wa askofu.

1. -Katika cheo ya upadri tuna tena cheo ya Mchunga-akiba (grade antique) yeye njo anachunga akiba ya Mitropolia.
2. Sakerarios, yteye ni mkuu wa utawalo wa Monasteri kubwa wa maandiko za kale za uzima ya utawa. Mume ao muke watalipiza kwa ruhusa ya askofu wakati wakifanya kosa. Yeye ni mwenye kusahihisha makosa yetu.
3. Skevofilakas. Huyu ni mchungaji wa vitu Vitakatifu vya Eklezya kisha ni yeye anaweka usafi mu Eklezya .
4. Khartofilakas: Padri huyu ni katibu wa askofu, ana na chumba cha kazi cha kuweka hati (dossier), cheti...Huyu ni mchungaji na wakaratasi yote).
5. Sakelin: Mkubwa wa monasteri ya watawa wanawake. yeye anawachunga wakati wote, katika uzima wao, na mapadri wanalipiza wenye kufanya mabaya.
6. Protekdikos: Huyu ni sawa msimamizi wa Mitropolia tena anasaidia mapadri ku baraza la hukumu kuu (Parquet).
7. Protosingelos: Hii ni cheo wanapatia mapadri ao Watawa wenye kuwa na ndoa, wanawakamata sawa wasaidizi wa pili wa askofu.
8. Ierokirikas (Muhubiri). Huyu padri kazi zake ni kuhubiri habari njema.

9. Arkieratikos epitropos. Mkubwa wa utawalo wa fasi moja ya Mitropolia. Mfano, padri Meletios sasa ni mkubwa wa fasi yetu huku katanga.

10.Protopresviteros: Ni cheo cha sifa cha mapadri, wanafanya kazi nzuri (kuhubiri, kusaidia maskini). Yeye eko juu ya mapadri wengine, wanavaa msalaba pa kilari yake.

## MAPADRI WATAWA

Cheo yao wanawaita Arkimandriti ni kusema: Cheo cha wakubwa wa nyumba ya Watawa (Monasteri). Nikusema huyu ni mkubwa ya nyumba ya watawa (monasteri). Wanamuchagua paka wale wanaishi ndani ya Monasteri na cheo yake ni mpaka mwisho ya uzima yake. Kama yeye wa pekee anataka kusimamisha kazi yake kwa ajili ya uzee ao ugonjwa yake fulani, watawa wa monasteri yake, wataweza kisha kuchagua mkubwa padri yao mwingine.

## CHEO YA ASKOFU

Waaskofu wote wanakaa pamoja na watawalo wa Eklezya wana cheo ya kwachana kwa mfano:

-Mitropoliti, Eksarkhos. Arkiaskofu. Cheo cha wakuu wa dini wa Mtaguso wa Maaskofu cheo ya Pape ilianza mu karne ya ine (Milele wa ine) Kama tunasema Mitropoliti nikusema eko na fasi yake ndani tunakuta askofu. na askofu weko wanatii Mitropolitis wao katika kazi yote ya utawalo. Mitropolia hawezi kufanya kazi ya utawalo bila askofu wake kujua vilevile. Mfano: Kujenga masomo...

-Mitropolitis hawezi kwenda kumwangalia Episkopos wake bila baraka ya huu askofu yake.

-Eksarkos ni kusema mkubwa wa dini anamupatia cheo hii kuwa mjumbe wa mkubwa wa dini juu ya kutengeneza mambo filani ya Eklezya.

-Huyu Mitropolitis na Eksarkos wana cheo cha mkubwa wa dini. Tangu karne ya ine (Milele wa ine) tuna cheo ya patriarkie cha dini ya Mashariki ni tano:

-Ya Roma.
-Konstantinopoli.
-Aleksandria ya Msiri.
-Antiokhia ya Siria.
Yerusalema.

Tuna na Patriarkie wa sasa: Mu inchi Rusia, Serbia, Rumania, Bulgaria  na Iviria (Georgia).

Eklezya ingine inachunga cheo ya mwisho ni arkiaskofu, kwa mfano Grekia, Kipros, Albania, Polonia, Filandia, Anglia, Franza, Amerika, Australia, Chekhia, Slovakia

Kwa ajili ya majivuno yake, wakuu wa dini ya Roma walipenda kutengeneza ma Patriarkat ingine. Ni kule kulitoka kugawanyika. Ni kusema makutano ya vatikan ya 1870 maaskofu wake 500 waliitika na kusema yeye ni chemchem ya Eklezya, mtu wasio na kosa na chemchem ya uwezo wote wa Eklezya, naye anabeba kiti ya Roho Mtakatrifu. Mafundisho hii ni matusi mbele ya Bwana Yesu Kristu.

**MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA (HELLAS)**
**1996**